


Fisi mlafi aliishi katika kijiji cha Mkosi.




Katika kijiji jirani, aliishi
Kobe mwoga. Fisi na Kobe
walikuwa marafiki.




Fisi alisikia kwamba kulikuwa na nyuki waliotengeneza asali tamu kuliko yote. Nyuki hao walisafiri mbali na mizinga yao mara moja kwa mwaka. "Lazima tuiplate ile asali nyuki watakapokuwa safarini," Fisi alimwambia Kobe.




Ingawa Kobe aliogopa kwenda, hakuwa na ujasiri wa kukataa. Asubuhi iliyofuata, Fisi na Kobe walianza safari yao. Fisi alienda kwa kasi huku Kobe akijikokota nyuma kwa woga.




Walipanda milima wakashuka kisha wakavuka mabonde. Waliuvuka mto mkubwa wakaendelea na safari yao wakiwa na nia ya kuifikia ile mizinga ya nyuki.




Hatimaye, waliona mizinga ya nyuki milimani kwenye miti. Fisi alikwenda kwa haraka. Kobe alikuwa tayari kuzirai kutokana na njaa na uchovu.




Fisi alipoufikia mzinga
mkubwa zaidi, alimwambia
Kobe, "Haraka! Panda juu
ya mti uuangushe mzinga
chini."



Kobe aling'ang'ana
kuupanda mti. Alipofanya
hivyo, aliangalia chini mara
kwa mara asije akaanguka.
Fisi alikasirishwa na kitendo
hicho akaanza kumpigia
Kobe kelele.




Kobe alipougusa mzinga,
alisikia sauti ya nyuki.
Kumbe walikuwa bado
ndani ya mzinga wao! Kobe
alishtuka akaanguka chini.



Mzinga wa nyuki ulimwangukia Kobe akafunikwana kufichwa na asali! Fisi alianza kuilamba ile asali. Lakini nyuki hawakufurahia kitendo hicho.




Nyuki walimuumma Fisi kila
sehemu ya mwili akaamua
kukimbilia usalama wake.
Hata hivyo, nyuki
walimfuata wakaendelea
kumooma.




Fisi aliteremka kutoka
mlimani, akavuka mto na
bonde. Nyuki waliendelea
kumuuma wakati huo wote.



Kobe naye alikuwa bado chini ya mzinga mkubwa. Hatimaye, kila kitu kilikuwa kimya. Kobe aligundua kwamba mzinga na asali vilikuwa vimekaukia mgongoni kwake.



Kobe alitambua kuwa
hakuhitaji tena kujificha
kichakani. Gamba jipya
alilopata lingeweza
kumkinga na hatari yoyote.



Fisi alikuwa amechoka na alijaa vidonda mwilini. Alizirai kabla kufika nyumbani. Alipoamka, aligundua kwamba mishale ya nyuki ilisababisha yeye kuwa na madoadoa kwenye ngozi yake.

Hivi ndivyo kobe alivyopata gamba lake ngumu
naye fisi akapata madoadoa kwenye ngozi yake.
Urafiki kati ya fisi na kobe uliisha.